# JARIDA LA MTANDAONI

NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED

# MEI MOSI 2024



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) tunaungana na **Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** katika kuadhimisha **Siku ya Wafanyakazi Duniani**.

**NHIF inatambua na kuthamini mchango wa Watumishi katika kuimarisha huduma.**

*"Nyongeza ya Mishahara ni Msingi wa Mafao Bora na Kinga Dhidi ya Hali Ngumu ya Maisha"*

# NHIF INAVYOTAMBUA NA KUTHAMINI MCHANGO WA WATUMISHI

- **Yaboresha huduma za Matibabu**
- **Umri wa wategemezi watoto waongezwa**
- **Kushirikiana na TUCTA katika maboresho mbalimbali**



MWAKA 2001, Watumishi wa Umma waliandika historia mpya ya kuwa wanachama namba moja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), na hii ni kutokana na ukweli kwamba Sheria iliyoanzisha Mfuko huu ililenga kundi la Watumishi peke yake.

Kutokana na mchango mkubwa kutoka Watumishi ambao umewezesha na umejenga uwezo na ustahimilivu wa NHIF katika utoaji wa huduma zake kwa wanachama mpaka hivi leo. Historia hii imejenga msingi mkubwa kwa NHIF kuthamini na kutambua mchango wa Watumishi kupitia Vyama vyao vya Wafanyakazi vikiongozwa na Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA).

Katika kuhakikisha Watumishi wa sekta ya Umma na Binafsi ambao ni asilimia 64 ya wanachama wa Mfuko wanaendelea kupata huduma bora, NHIF imekuwa ikiishirikisha TUCTA katika maboresho mbalimbali ambayo yameendelea kufanyika katika huduma ili kuepukana na changamoto au malalamiko yanayoweza kujitokeza.

Ushirikishwaji wa kundi hili ni mkubwa ni kutokana na ukweli kwamba , idadi kubwa ya wanufaika wa NHIF inatokana na kundi la Watumishi hivyo ni wadau wakubwa wa Mfuko katika mabadiliko yoyote yanayojitokeza.

Wakati Mfuko unaanza mwaka 2001, Kitita cha mafao cha Mfuko kilijumuisha huduma chache ikilinganishwa na maboresho makubwa yaliyofanywa sasa. Maboresho ya sasa yamezingatia hali halisi ya mahitaji ya wanachama, uwepo wa magonjwa ambayo awali hayakuwepo, teknolojia tibailiyopo kwa sasa.

Tukiangazia maboresho makubwa ambayo yamefanyika chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mengi na ambayo yameleta manufaa makubwa kwa wafanyakazi wa sekta ya Umma na Binafsi. Maboresho hayo ni pamoja na;-

- **Kuongezwa umri wa Mtoto mtegemezi wa Mwanachama**

Katika kuhakikisha Watumishi wanapata huduma bora, Mei 1, 2021 Mhe. Rais akiwa katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi, aliagiza kuongezwa kwa umri wa Watoto Wategemezi wa wanachama kutoka miaka 18 hadi miaka 21.

Hatua hii ilikuwa ni mafanikio makubwa kwa Serikali ya Awamu ya Sita na kwa Watumishi kwa kuwa ililenga kupunguza mzigo wa gharama za matibabu kwa watoto wao ambao awali ukomo ulikuwa ni miaka 18.

- **Kitita kipya cha Mafao cha Mfuko cha Mwaka 2023**

Ili kwenda sambamba na bei halisi ya soko la bidhaa za afya na maendeleo ya sayansi tiba pamoja na uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Afya uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita hususan katika ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za matibabu, uwekezaji wa Vifaa tiba vya kisasa, uwekezaji wa Wataalam na Miundombinu, Mfuko ulifanya marejeo ya Kitita chake cha Mafao cha mwaka 2016 na kuja na kitita kipya cha Mafao cha Mwaka 2023 kilichoanza kutumika tarehe 01 Machi 2023.

Manufaa makubwa yaliyomo ndani ya Kitita cha Mafao cha mwaka 2023 kwa wanachama wake ni pamoja na ;-
Kusogeza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchi kuanzia Hospitali za ngazi mkoa na Kanda, kuondoa usumbufu wa kukosa baadhi ya dawa na huduma nyingine, ongezeko dawa mpya 254 ambazo awali wanachama walilazimika kutoa fedha taslimu kwakuwa hazikuwa sehemu ya Kitita cha mwaka 2016, kupunguza gharama za matibabu nchini na kuwezesha wananchi wasio na bima ya afya kumudu gharama hizo.

Manufaa mengine ni kuweka usawa wa ada ya usajili kwa madaktari wenye elimu na taaluma zinazofanana hivyo kuondoa malalamiko, kuwaepusha wanachama kuendelea kutumia dawa zisizo na matokeo chanya hivyo kuwaepusha na magonjwa yasiyoambukizwa kutokana



na usugu wa dawa husika pamoja na kuwaepusha watoa huduma na makato yasiyo ya lazima kwakuwa utoaji wa huduma utazingatia miongozo ya Tiba na Orodha ya Taifa ya dawa Muhimu.

Mbali na maboresho haya, Mfuko pia umepanua huduma zake kwa kuanzisha fursa kwa wananchi kujiunga na bima ya afya kupitia vifurushi vya Bima ya Afya vya Najali Afya, Wekeza Afya na Timiza Afya ambavyo vimezingatia umri, ukubwa wa familia, aina ya huduma na gharama halisi za matibabu atakazochagua mwanachama.

- **Ushirikiano wa NHIF na TUCTA**

Katika utekelezaji wa majukumu yake NHIF, imekuwa ikishirikiana na TUCTA hususan katika mabadiliko mbalimbali ya kihuduma kwa lengo la kundi hilo kujua mabadiliko husika lakini pia kushauri namna bora ya utekelezaji wa maboresho hayo.

Katika kikao cha pamoja kilichofanyika Aprili 26, mwaka huu, NHIF na TUCTA kwa pamoja walikubaliana kushirikiana katika utoaji wa elimu juu ya huduma zinazotolewa na Mfuko hususan katika maeneo ya Wajibu wa Wanachama na haki zao pamoja na wajibu wa Waajiri katika kuwasilisha michango ya Watumishi wao kwa wakati.

Makubaliano haya ya ushirikishwaji yanakwenda kujenga msingi imara wa mahusiano na kuondoa malalamiko mengi ambayo yamekuwa yakisababishwa na baadhi ya wanachama kukosa elimu katika huduma husika.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bw. Bernard Konga amewahakikishia Watumishi wa Umma na Binafsi kuwa Mfuko utaendelea kutoa huduma bora, kuboresha huduma kulingana na mahitaji yaliyopo na kwa kuzingatia hali ya ustahimilivu wa Mfuko.



Naye Rais wa TUCTA Bw. Tumaini Nyamhokya ameweka wazi kuwa Shirikisho hilo liko tayari kushirikiana na NHIF ili kuhakikisha Mfuko unazidi kuwa imara na unahudumia vizazi na vizazi kwa kuwa Mfuko huo ni nguzo kubwa katika utoaji wa matibabu.

**Uhakika wa Matibabu kwa Wote**